

# Uwezo Tanzania

## Kitabu cha Majaribio



## Kitabu cha Majaribio 2022





**SETI 1****Kiswahili****Silabi**

hu zo da pi  
ne tu yo we  
vi sha

- Mtoto achague na kusoma silabi zozote 5. Kati ya hizo nne ziwe sahihi.

**Maneno**

muwa lori homa  
kiti chana posho  
jani wale kesi  
soma

- Mtoto achague na kusoma maneno 5. Kati ya hayo manne yawe sahihi.

**Aya 1**

Mama alienda sokoni jana asubuhi.  
Alirudi jioni na dawa nzuri ya  
meno. Sisi hupenda sana kupiga  
mswaki. Meno yetu ni safi sana.

**Aya 2**

Jana usiku upepo mkali ulivuma.  
Upepo huo mkali uliezua nyumba  
yetu. Majirani wengi walikuja  
kuokoa maisha yetu. Hakika  
nimejua ujirani mwema ni mzuri.

- Mtoto achague aya yoyote na asome kwa usahihi.

**SETI 1****Kiswahili****Hadithi**

Mgasa anasoma katika shule ya msingi Juhudi. Yeye anapenda sana kucheza mpira wa miguu. Kila siku jioni Mgasa hufanya mazoezi. Pia, hucheza mpira na wenzake.

Siku moja kulikuwa na mashindano. Timu ya Juhudi na timu ya Sesele zilipangwa kuanza. Siku ya mashindano ilipofika ziliingia uwanjani. Timu ya Juhudi ilishinda kwa magoli matatu. Kati ya hayo Mgasa alifunga magoli mawili. Timu ya Sesele haikufunga hata moja. Timu ya Juhudi ilifurahi sana.

Maswali









1. Timu ya Sesele ilifunga Magoli mangapi?
2. Kwanini Mgasa anafanya mazoezi kila siku jioni?

- Mtoto asome hadithi kwa usahihi. Mtoto aliyesoma kwa usahihi ajibu maswali yote mawili.

# SETI 1

## Hisabati

### Taja Idadi

	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>

- Mtoto ahesabu mafungu matano (5) angalau manne (4) awe sahihi

### Utambuzi wa Namba

11	24	38	45
69	77	80	92

- Mtoto asome namba tano (5) angalau nne (4) ziwe sahihi

### Jaza namba zilizokosekana katika jedwali hili

11	12			15		17	
	20		22		24		26
27		29		31		33	

- Mtoto ataje namba tano (5) zilizokosekana, angalau nne (4) ziwe sahihi

# SETI 1

## Hisabati

### Kujumlisha Namba

$$\begin{array}{r} 25 \\ + 16 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 38 \\ + 56 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 47 \\ + 28 \\ \hline \end{array}$$

- Mtoto ajumlisha mafungu matatu (3) angalau mawili(2) yawe sahihi

### Kuzidisha Namba

$$2 \times 2 = \quad 5 \times 1 = \quad 3 \times 3 =$$

- Mtoto afanye mafungu matatu (3) angalau mawili(2) yawe sahihi

### Kutoa Namba

$$\begin{array}{r} 71 \\ - 42 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 72 \\ - 39 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 78 \\ - 39 \\ \hline \end{array}$$

- Mtoto atoe mafungu 3 angalau 2 yawe sahihi.

### Kugawanya Namba

$$4 \div 2 = \quad 5 \div 1 = \quad 2 \div 1 =$$

- Mtoto afyanye hesabu 3 angalau 2 ziwe sahihi.

**SETI 2****Kiswahili****Silabi**

la me su ka  
di wo bu fi  
ze cho

- Mtoto achague na kusoma silabi 5. Kati ya hizo 4 ziwe sahihi.

**Maneno**

mama ruka hamu  
kitu cheza pasha  
jana wali kosa  
somo

- Mtoto achague na kusoma maneno 5. Kati ya hayo manne yawe sahihi

**Aya 1**

Nyumbani kwetu kuna maua.  
Maua ni mazuri na huvutia sana.  
Vipepeo wengi hutua juu yake. Mimi  
hupenda kuwaona vipepeo wakitua  
na kuruka.

**Aya 2**

Ana na Rehema ni marafiki wazuri.  
Wote wanasoma darasa la pili. Wao  
husoma pamoja kila siku kwa bidii.  
Wote wawili wanajua kusoma vizuri

- Mtoto achague aya yoyote na asome kwa usahihi

**SETI 2****Kiswahili****Hadithi**

Mimi na baba tulienda mbuga ya Mikumi. Hii ni mbuga ya wanyama iliyoko mkoani Morogoro. Huko mbugani tuliwaona wanyama wengi sana. Tuliwaona twiga, nyati, tembo, simba na swala. Twiga wote ni wazuri na wanavutia zaidi. Mimi niliwapenda sana twiga.

Mimi nilifurahi sana kuwaona wanyama mbalimbali. Tuliporudi nyumbani nilisimulia mambo yote niliyoyaona huko. Mama akaniambia kuwa tembo huwavutia sana watalii. Watalii wengi huja Tanzania kuwaona tembo. Hakika sisi tulifurahia sana safari hiyo.

**Maswali**

1. Mbuga ya wanyama ya Mikumi iko mkoa gani?
2. Kwanini safari ya Mikumi ilikuwa ya kufurahisha?









- Mtoto asome hadithi kwa usahihi. Mtoto aliyesoma kwa usahihi ajibu maswali yote mawili



**SETI 2**

**Hisabati**

**Taja Idadi**

	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>
	<input type="text"/>

- Mtoto ahesabu mafungu matano (5) angalau manne (4) awe sahihi

**Utambuzi wa Namba**

14	29	36	57
66	74	88	93

- Mtoto asome namba tano (5) angalau nne (4) ziwe sahihi

**Jaza namba zilizokosekana katika jedwali hili**

21	22			25		27	
	30		32		34		36
37		39		41		43	

- Mtoto ataje namba tano (5) zilizokosekana, angalau nne (4) ziwe sahihi

## SETI 2

### Hisabati

#### Kujumlisha Namba

$$\begin{array}{r} 65 \\ + 16 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 19 \\ + 67 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 37 \\ + 24 \\ \hline \end{array}$$

- Mtoto ajumlisha mafungu matatu (3) angalau mawili(2) yawe sahihi

#### Kuzidisha

$$3 \times 2 = \quad 5 \times 1 = \quad 4 \times 3 =$$

$$4 \times 2 = \quad 6 \times 3 = \quad 5 \times 4 =$$

- Mtoto afanye mafungu matatu (3) angalau mawili(2) yawe sahihi

#### Kutoa Namba

$$\begin{array}{r} 52 \\ - 29 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 63 \\ - 24 \\ \hline \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 53 \\ - 35 \\ \hline \end{array}$$

- Mtoto atoe mafungu 3 angalau 2 yawe sahihi.

#### Kugawanya

$$9 \div 3 = \quad 8 \div 2 = \quad 4 \div 2 =$$

- Mtoto afyanye hesabu 3 angalau 2 ziwe sahihi.

## SWALI LA ZIADA

**A. Je mtoto anaweza kuonesha bendera ya taifa la Tanzania?**

1.



2.



3.



**B. Je mtoto anaweza kutaja muda sahihi (saa na dakika) kwenye picha?**



## **Elimu Bora Tanzania inawezekana, Timiza wajibu wako!**

---



Uwezo Tanzania  
Kinondoni Road | P.O. Box 8259 | Dar es Salaam | Tanzania  
T: +255 735 041 143 |  
E: [info@uwezotanzania.or.tz](mailto:info@uwezotanzania.or.tz) | Web: [www.uwezotanzania.or.tz](http://www.uwezotanzania.or.tz)